

**SALAMU ZA MKUU WA MKOA KATIKA  
MAADHIMISHO YA SHEREHE YA WAUGUZI  
DUNIANI KATIKA MKOA WA RUKWA  
YALIYOFANYIKA SUMBAWANGA TAREHE 12  
MEI, 2017**

**Mwenyekiti wa CCM Mkoa,**

**Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya,**

**Mganga Mkuu wa Mkoa**

**Muuguzi Mkuu wa Mkoa,**

**Mwenyekiti wa Chama cha Wauguzi Mkoa wa  
Rukwa,**

**Viongozi wa TANNA kutoka katika matawi yote,**

**Wauguzi,**

**Watumishi wote wa Sekta ya Afya,**

***Ndugu Mwenyekiti wa Chama cha Wauguzi Mkoa wa Rukwa,***

Leo ni siku ambayo Wauguzi Duniani kote wapo katika maadhimisho ya siku ya Wauguzi ambapo pia ninyi katika Mkoa wa Rukwa mnashiriki. Tunashukuru sana kwa maamuzi yenu ya kutushirikisha sote tuliopo hapa na kunipa mimi heshima ya kuwa mgeni rasmi.

Nipende kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe Mwenyekiti wa Chama cha Wauguzi na wenzako wote katika Mkoa wa Rukwa kwa kazi nzuri ya uuguzi ambayo mnaendelea kuifanya katika maeneo mbalimbali yanayohitaji uwepo wenu. Kila mmoja wetu katika Mkoa anatambua umuhimu wenu na hata ninyi mnatambua umuhimu wenu katika Hospitali zetu.

***Ndugu Mwenyekiti wa Chama cha Wauguzi Mkoa wa Rukwa,***

Nachukua nafasi hii vilevile kuwashukuru kwa ushirikiano wenu mnaouonesha kwa madaktari, wagonjwa na wadau wengine wote katika Sekta ya Afya ndani ya Mkoa huu.

Niwapongeze kwa kuendeleza kwa moyo wa dhati kabisa misingi yote ya mwanzilishi wa uuguzi Bi. Florence Night Ngale. Mwanzilishi huyu inaonesha katika historia kwamba ni mama aliyejitoa kikamilifu katika hali ngumu na kutoa huduma za uuguzi. Ni matumaini yangu nanyi hamtatofautiana na mama huyo wa mfano. Kazi yenu tunaamini ni ya wito kwa kizalendo na imani.

***Ndugu Mwenyekiti wa Chama cha Wauguzi Mkoa wa Rukwa,***

Kauli Mbiu yenu ya Mwaka huu inasema  
***“WAUGUZI NI MBIU YA KUYAFIKIA MALENGO***

**ENDELEVU YA MILENIA".** Endeeleni kutoa huduma kama kauli mbiu hiyo ili tuweze kufikia malengo ya milenia ya kupunguza Vifo vya Akina Mama wajawazito, watoto pamoja na UKIMWI kwa kutoa huduma kwa weledi, kujituma, upendo, huruma na kuzingatia taaluma yenu. Endeeleni kutoa elimu kwa akina mama au wasichana wanaojifungua katika umri mdogo kwa kuwapa elimu juu ya lishe bora kwa watoto ili kuepukana na Udumavu. Na hii ni kutokana na kuwa ninyi wauguzi mna uelewa mpana na mchango mkubwa sana katika Mkoa na jamii kwa ujumla. Tunategemea kusonga mbele kiuchumi. Na hii itawezekana kama wauguzi mtatoa elimu kwa jamii juu ya masuala hayo.

***Ndugu Mwenyekiti wa Chama cha Wauguzi Mkoa wa Rukwa,***

Napenda kuisitiza kwamba, Halmashauri wanatakiwa kununua dawa na vifaa tiba ili wauguzi waweze kutoa huduma zao wakiwa huru ili

kuepuka migogoro inayoweza kutokea kati yao na wagonjwa.

Natoa agizo Wakurugeni wote wa Halmashauri wahakikishe pesa wanazoletewa na Serikali kwenye mfuko wa pamoja wa afya (Basket Fund) hazitumiki kwa kazi nyingine yoyote zaidi ya kununua dawa na vifaa tiba.

Wakurugenzi wa Watendaji chini yao wahakikishe wanasimamia wananchi kujiunga na mfumo wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF). Hali kadhalika kusimamia makusanyo ya papo kwa papo kwa kutumia mashine za kielektroniki na kupelekwa benki.

***Ndugu Mwenyekiti wa Chama cha Wauguzi Mkoa wa Rukwa,***

Katika risala ya wauguzi kero mbalimbali zimeainishwa nami nataka nwahakikishie

nimeyasikia na ningependa mnipe nafasi ya kwenda kuyafanyia kazi kwa kushirikisha watendaji wa sehemu mbalimbali ambao wanahusika kuyasimamia maslahi ya watumishi hao isipokuwa napenda niwakumbushe tena wauguzi wetu kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ilikutana na mambo mengi ambayo ilibidi kusimamisha stahiki mbalimbali kutokana na udanganyifu, kutokana na hewa, kutokana na vyeti feki n.k. ambayo wote tumeona hatua zinazochukuliwa. Haya yote yanalenga kuhakikisha kwamba wanaonufaika ni wale ambao wanastahili. Nawaomba muwe na subira pia.

***Ndugu Mwenyekiti wa Chama cha Wauguzi Mkoa wa Rukwa,***

Natambua na ninahitaji iwe hivyo wauguzi wetu wapate sare, wapandishwe vyeo, wapate stahiki za likizo, matibabu na hata makazi hususani katika vituo vile vitakavyojengwa vijijini.

***Ndugu Mwenyekiti wa Chama cha Wauguzi Mkoa wa Rukwa,***

Natambua kwamba matatizo mengi ya wauguzi yapo kwenye Halmashauri zetu. Nawaagiza Wakurugenzi waone umuhimu wa kuwahudumia ipasavyo wauguzi kwa kulinda na kutekeleza stahiki zao ikiwepo la kuwalipa fedha kwa ajili ya sare na sio kuwapa vitambaa.

Mwisho napenda kuwaasa wauguzi waendeleo kuwa waaminifu na hasa katika dawa na vifaa tiba katika maeneo yao ya kwao. Naamini wauguzi wetu wa sasa ni waguzi wa mabadiliko.

Nawatakia maadhimisho mema ya Sherehe ya Wauguzi Duniani.

Zelote Stephen Zelote

**MKUU WA MKOA WA RUKWA**

